**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

**Mheshimiwa Spika,**
Awali ya yote, hatuna budi kumshukuru Allah Subuhanahu Wataala kwa kutujaalia uhai pamoja na afya njema, ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kiujumla. Ninamuomba Allah Mtukufu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, napenda kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako wa Baraza hili, ambao ni Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa. Namuomba Allah awazidishie busara na hekma katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika Muhimili huu muhimu wa Dola.

Vile vile, pongezi za dhati ziende kwa Uongozi nzima wa Wizara Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi zao kubwa na mashirikiano wanayotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu. Kamati inawaomba waongeze juhudi katika kutekeleza na kusimamia kazi zao ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa kuyatekeleza kwa mwaka husika wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa hakika, itakuwa si busara iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba kuchukua fursa hii kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| *9.* | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**
Kanuni ya *108(15)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa mapendekezo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na Wizara husika kujadili utekelezaji huo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa hivyo, baada ya utangulizi huo sasa naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo na Ushauri wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambapo jumla ya mapendekezo yalikuwa 43 tuliyoyawasilishwa kwa Wizara na tunashukuru yote yameweza kupatiwa majibu ya kina.

## CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati katika kufuatilia majukumu yake ilibahatika kutembelea Skuli ya Biashara ilioko Chwaka na kubaini changamoto mbali mbali za kiutendaji ikiwemo uhaba wa Bajeti, ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, uchakavu wa majengo, ukosefu wa usafiri pamoja uwepo wa Dakhalia moja yenye mchanganyiko wa wanafunzi wa kike na kiume.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na changamoto hizo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuliangalia upya suala la uunganishaji wa Vyuo hivi, kwani Kamati imegundua tangu kuunganishwa kwake baadhi ya Skuli na Vyuo vimekuwa vinadhorota kiutendaji hali inayopelekea hadhi na haiba ya fani zilizokuwa zikitolewa kupungua na hata nyengine kutokusomeshwa tena Zanzibar na kusababisha wataalam wanaohitajika kukosekana.

## KITENGO CHA ELIMU MJUMUISHO NA STADI ZA MAISHA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Marais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kufanikisha ujenzi wa Skuli za Kisasa katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba kupitia fedha za Ahuweni za UVIKO 19. Kamati, ina matumaini makubwa kwamba majengo hayo ya kisasa yatakuwa na vifaa vya kisasa vyenye kurahisisha masuala ya kujifunza na kufundishia kwa wanafunzi wetu kuanzia Elimu ya Maandalizi, Msingi na hata Sekondari. Aidha, Serikali itajiandaa mapema kuweza kupata walimu wa kutosha kwenye skuli hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, Kamati inafurahishwa na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali yetu ya Zanzibar kwa kujenga Skuli mbili za ghorofa za Elimu Mjumuisho kwa Unguja na Pemba kupitia fedha hizo za Ahweni za UVIKO 19. Hatahivyo, Kamati imebaini baada ya ujenzi huo kukamilika changamoto kubwa itakayojitokeza ni uhaba wa walimu wataalamu waliobobea katika fani hizo. Kwa sasa walimu waliopo wanakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ukosefu wa posho maalum, uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, ukosefu wa Muundo wa Utumishi kwa Walimu wa Elimu Mjumuisho pamoja na uchache wa walimu walisomea Masomo ya Elimu Mjumuisho kwa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu, inapendekeza kwa Serikali katika masuala ya ajira za walimu basi ni vyema wakapewa kipaumbele walimu wanaojitolea kwa muda mrefu katika skuli zetu pamoja na wale wenye sifa ambao walioomba na watakaoomba katika nafasi za ajira zinazoendelea kutolewa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kukamilika kwa skuli hizo kutafanikisha Dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane ya kupunguza msongamano wa idadi ya wanafunzi ndani ya madarasa, hivyo kupelekea wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri.

## UONGOZI NA UTAWALA

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inaipongeza Tume ya Kurekebisha Mtaala wa Elimu Tanzania kwa kukutana na Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutoa maoni, ushauri pamoja na mapendekezo kuhusu uboreshaji wa Mtaala wa Elimu Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa umuhimu wa Elimu Tanzania nzima, Kamati inaiomba Kamati au Tume ya Kurekebisha Mtaala wa Elimu Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba ikutane na Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kutoa maoni, ushauri pamoja na mapendekezo ili Mtaala wetu wa Elimu Tanzania kwa maana ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa ujumla uwe bora zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**
Hitimisho, Kamati inatoa shukurani za dhati kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………………

Mhe. Mohamed Ahmada Salum,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**